

Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

[الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

**“Wale ambao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqarah: 156]
(Imetafsiriwa)**

Kwa nyoyo zilizo jaa imani na kukubali Qadhaa ya Mwenyezi Mungu Subhanahu Wa Ta’ala, na kwa macho yaliyo jaa machozi, Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Sudan inamuboleza aliye samehewa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu:

Hussein Hamed Fadl Al-Mawla (Mahejin)

Mmoja wa wanachama wake aliyefanya kazi ya kuregesha maisha kamili ya Kiislamu, kupitia kusimamisha Dola ya Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume, aliyefariki kutokana na ajali ya gari. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) amrehemu, amsamehe madhambi yake, amkirimu, ajaaliye mashukio yake yawe mapana, na aimiminie baraka familia yake na kizazi chake, na aturuzuku sisi na kaka zake na dada zake katika Da'wah, pamoja na familia yake, subira na faraja njema.

[إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea”

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
Wilayah Sudan**